JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU HUDUMA ZITOLEWAZO NA MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA (TACAF)

MEI, 2024 - TOLEO LA KWANZA

## NENO LA AFISA MTENDAJI MKUU

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) umeandaa kitabu hiki kwa ajili ya kujibu maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa mara kwa mara na wadau wetu. Lengo ni kuongeza uelewa kwa wateja wetu kuhusu huduma tunazotoa na kuwawezesha kuzifikia kwa urahisi wakiwa popote. Ahadi yetu kwa wadau wetu siku zote ni kuwapatia huduma bora na kwa wakati.

Kitabu hiki ni sehemu ya jitihada za kutengeneza mazingira rafiki kwa wadau wetu ili waweze kupata huduma kwa urahisi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo. Ndani ya kitabu hiki, wadau wetu watapata majibu ya maswali yote ambayo yamekuwa yakiulizwa kuhusu vigezo na taratibu za kuwasilisha maombi ya mikopo, vigezo vinavyotumika kupata mikopo au kupata mafunzo yatakayowasaida waweze kutimiza vigezo vya kupata huduma.

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa utaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya kuboresha kitabu hiki kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuweza kufikia kiwango cha matarajio yao. Vilevile tunatarajia kitabu kitaweza kutoa majibu ambayo yataweza kuwasaidia katika kuandaa maombi na kuyawasilisha katika mamlaka husika. Ni imani yangu kwamba, kwa kupitia kitabu hiki, malalamiko kuhusu changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza wakati wa kuandaa na kutuma maombi ya huduma mbalimbali yatapungua, na kuwa chachu ya wadau wengi zaidi kupata huduma zetu.

NYAKAHO MTURI MAHEMBA

AFISA MTENDAJI MKUU

**MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA**

# SURA YA KWANZA

## UFAHAMU KUHUSU MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

1. **Je, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ni taasisi ya Serikali au Binafsi?**
   Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ni taasisi ya umma inayosimamiwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Imesajiliwa kwa Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 Septemba, 2020.

2. **Ni nini lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu?**
   Lengo kuu la Mfuko ni kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili zijiendeshe kibiashara, kutengeneza ajira na kuchangia pato la Taifa.

3. **Je, Mfuko unahudumia maeneo gani katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa?**
   Mfuko unahudumia maeneo matano (5) ambayo ni:-
   (a) Sanaa za Maonyesho - Ushereheshaji, Mapambo, Upishi wa Keki n.k
   (b) Sanaa za Ufundi – Uchongaji, Uchoraji, Ufumaji, Ushonaji, Urembo, Uchapishaji n.k
   (c) Filamu – Uandaaji wa Maudhui, Uzalishaji wa Filamu, Usambazaji n.k
   (d) Muziki - Singeli, Injili, Kaswida, Rege, Kizazi Kipya, Dansi, Taarabu, Usambazaji n.k
   (e) Lugha na Fasihi – Uandishi wa makala, uchapishaji n.k

4. **Je, Mfuko unahudumia wadau gani?**
   Mfuko wa unahudumia wadau wafuatao:-
   a) Watu binafsi wanaojishughulisha na kazi za Utamaduni au Sanaa, waliosajiliwa/kutambulika katika mamlaka za Serikali zinazosimamia kazi za Utamaduni na Sanaa;
   b) Vikundi vya Utamaduni na Sanaa;
   c) Vyama vya Utamaduni na Sanaa;
   d) Mashirikisho ya Utamaduni na Sanaa;
   e) Makampuni yanayojishughulisha na Utamaduni & Sanaa;
   f) Vituo vya elimu na mafunzo vinavyoshughulika na Utamaduni na Sanaa; na
   g) Asasi za kiraia zinazoshughulika na masuala ya Utamaduni na Sanaa.

5. **Je, ninaweza kupata wapi taarifa kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa?**
   Unaweza kupata taarifa za Mfuko kupitia maeneo yafuatayo:-
   a) Maafisa Utamaduni walioko katika ngazi za Halmashauri na Mikoa;
   b) Kupitia Ofisi zake zilizopo Jengo la Utumishi, Kivukoni- Dar Es- Salaam
   c) Kupitia matawi yote ya Benki ya CRDB na NBC nchi nzima
   d) Kupitia Tovuti ; www.tacaf.go.tz; Mitandao ya kijamii; *mfukotamadutz*

# SURA YA PILI

## HUDUMA ZA MIKOPO

1. **Je, Ni Huduma gani zitolewazo na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa?**
   Mfuko unatoa huduma za aina tatu ambazo ni Mikopo, Mafunzo na Ruzuku.

2. **Je, Mfuko unatoa mikopo ya aina ngapi?**
   Mfuko unatoa mikopo ya aina tatu ambayo ni *Mikopo ya Vifaa*, *mikopo ya uendeshaji na mikopo ya dharura*.

3. **Je, kuna tofauti gani kati ya mikopo ya vifaa, mikopo ya uendeshaji na mikopo ya dharura?**
   - **Mikopo ya vifaa:** Hutolewa kwa ajili ya kumuwezesha Mteja Kununua vitendea kazi vya kuzalishia kazi za Utamaduni na Sanaa kama vile vifaa vya Studio, magari ya kubebea wasanii wanaoendWa kurekodi kazi za Sanaa, vyombo vya muziki wa Bendi n.k
   - **Mikopo ya uendeshaji:** Hutolewa kwa ajili ya kuwezesha uendeshaji wa kazi za Utamaduni au Sanaa kama vile matamasha, mashindano, uzinduzi, utangazaji, pango n.k
   - **Mikopo ya dharura:** Hutolewa ajili ya kumuwezesha Mteja kujikimu wakati wa safari za kuandaa au kufanikisha kazi za Utamaduni au Sanaa mfano Msanii anapopata ziara ya kusafiri ndani na nje ya nchi kikazi.

4. **Je, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unatoa mikopo moja kwa moja kwa wasanii?**
   Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unafanya kazi kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB na NBC. Hivyo, Mfuko unatumia Taasisi hizi kwa ajili ya kutoa huduma za mikopo kwa walengwa.

5. **Je, Mfuko unawafikiaje wasanii wa mikoani?**
   Mfuko unawafikia wasanii walioko mikoani kupitia matawi ya Benki ya NBC na CRDB, Maafisa utamaduni walioko katika ngazi za Halmashauri na Mikoa na kupitia Vyama vya Utamaduni na Sanaa nchi nzima.

6. **Je, Wasanii wakitaka mikopo wanawasilisha maombi yao moja kwa moja katika Benki ya NBC na CRDB?**
   Wateja wakitaka mikopo wanatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe au kupitia sanduku la Posta au moja kwa moja katika Ofisi za Mfuko.

7. **Je, ni kwanini Mfuko unashirikiana na Benki ya CRDB na NBC katika utoaji wa mikopo?**
Mfuko unashirikiana na Benki ya NBC na CRDB ili kuongeza thamani ya utoaji wa huduma ikiwa pamoja na kutumia miundombinu ya matawi yao, wataalamu wenye ujuzi na uzoefu katika upembuzi wa miradi na usimamizi wa mikopo.

8. **Je, Msanii anaweza kuomba mkopo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za Kilimo au sekta nyingine?**
Mfuko unatoa mikopo ili kuendeleza shughuli za Utamaduni na Sanaa tu, Sio sekta nyingine nje ya Utamaduni na Sanaa.

9. **Je, kiwango gani cha Mikopo kinachotolewa na Mfuko?**
Kiwango cha Mkopo kinaanzia Shilingi Laki mbili (SHS, 200,000) hadi Shilingi Milioni Mia Moja (Shs 100,000,000/=).

10. **Je, riba ya mikopo ni asilimia ngapi?**
Riba ya mikopo inayotolewa na Mfuko ni asilimia 9 (9%) kwa mwaka inayotozwa katika salio la Mkopo (*Declining/Reducing Balance Method*)

11. **Je, Muda wa marejesho ya mkopo ni miaka mingapi?**
Muda wa marejesho ya mikopo ni miezi Ishirini na Nne (Miaka Miwili)

12. **Je, kuna muda wa rehema (grace period) katika mikopo inayotolewa na Mfuko kwa kushirikiana na Benki ya NBC na CRDB?**
Muda wa rehema ni hadi miezi mitatu (3) hata hivyo, muda huu utategemea na aina ya mradi ulioombewa mkopo.

13. **Je, Msanii anatakiwa kuwasilisha dhamana ili aweze kupata mkopo?**
Takwa la uwasilishaji wa dhamana kwa Msanii linategemeana na kiwango cha Mkopo kilichoombwa na kuidhinishwa mfano: -
   a) **Kuanzia Shilingi Laki Mbili (Shilingi 200,000) hadi Shilingi Milioni Kumi na Tano (Shilingi 15,000,000)** - Hakuna takwa la uwasilishaji wa dhamana.
   b) **Kuanzia Shilingi Milioni 15$^{+}$ hadi Shilingi Milioni 30** - Mwombaji atatakiwa kuwasilisha dhamana yenye thamani ya asilimia 20 ya kiwango cha Mkopo kitakachoidhinishwa.
   c) **Kuanzia Shilingi Milioni 30$^{+}$ hadi Shilingi Milioni 50**: Mwombaji atatakiwa kuwasilisha dhamana yenye thamani ya asilimia 30 ya Kiwango cha mkopo kitakachoidhinishwa.
   d) **Kuanzia Shilingi Milioni 50$^{+}$ hadi Shilingi Milioni 100**; Mwombaji atatakiwa kuwasilisha dhamana yenye thamani ya asilimia 50 ya kiwango cha mkopo kitakachoidhinishwa.

**14. Je, Msanii binafsi, kikundi au Kampuni inaweza kunufaika na mikopo itolewaji na Mfuko kwa kushirikiana na Benki?**

Mfuko unatoa mikopo kwa Msanii Binafsi, kikundi na Kampuni ili mradi vijishughulishe na kazi za Utamaduni/ Sanaa.

**15. Je, mahitaji gani yanahitajika ili Msanii binafsi aweze kuwasilisha maombi yake ya mkopo kwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha maombi ya mkopo kwa Msanii binafsi

a) Barua ya maombi ya mkopo;
b) Fomu ya maombi ya mkopo;
c) Andiko la Mradi;
d) Barua ya utambulisho wa makazi na eneo la biashara kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji;
e) Kitambulisho cha Taifa/Hati ya Kusafiria/Leseni ya Udereva;
f) Cheti cha usajili kutoka Taasisi inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya mwombaji kwenye Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa kama BASATA au Bodi ya Filamu;
g) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN);
h) Barua ya uthibitisho kuwa Mwombaji ni mwanachama wa umoja wowote ikiwamo Shirikisho; Chama au Kikundi kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa na ametambulishwa kwa maandishi na umoja huo;
i) Picha mbili za mkopaji na Mweza wake kama yupo;
j) Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama yapo;
k) Uthibitisho wa utekelezaji wa kazi za Sanaa/Utamaduni na mzunguko wake kupitia Benki Statement au miamala ya simu; na
l) Ankra Kifani (endapo mkopo ni wa vitendea kazi).

**16. Je, mahitaji gani yanahitajika ili kikundi kiwasilishe maombi yake ya mkopo kwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha maombi ya mkopo kwa kikundi cha Sanaa

a) Barua ya maombi ya mkopo;
b) Fomu ya maombi ya mkopo;
c) Andiko la Mradi;
d) Picha mbili za viongozi wa Kikundi;
e) Nakala ya hati ya usajili;
f) Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanachama wa kikundi wenye ajenda ya maombi ya mkopo;
g) Leseni ya Bishara;
h) Katiba ya kikundi;
i) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN);
j) Barua ya utambulisho wa makazi na eneo la biashara kutoka kwa

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji kwa Viongozi wa Kikundi

k) Barua ya uthibitisho kuwa kikundi ni mwanachama wa Umoja wowote ikiwamo Shirikisho; Chama kiichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa na ametambulishwa kwa maandishi na umoja huo;
l) Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama yapo
m) Uthibitisho wa utekelezaji wa kazi za Sanaa/Utamaduni na mzunguko wake kupitia Benki Statement au miamala ya simu; na
n) Ankra Kifani (endapo mkopo ni wa vitendea kazi)

### 17. Je, mahitaji gani yanahitajika ili Kampuni iwasilishe maombi yake ya mkopo kwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa?

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha maombi ya mkopo kwa Kampuni inayofanya kazi za Sanaa

a) Barua ya maombi ya mkopo;
b) Fomu ya maombi ya mkopo;
c) Andiko la Mradi;
d) Taarifa ya benki kuonyesha mtiririko wa fedha/Bank Statement ya mwaka moja;
e) Hati ya Usajili;
f) Leseni ya biashara;
g) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN);
h) Katiba ya Kampuni (Memorandum and Article of associations);
i) Maazimio ya Bodi/ Board Resolution;
j) Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanamiliki wa Kampuni ukionesha mahitaji ya mtaji na kuafikia kuomba mkopo;
k) Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama yapo;
l) Cheti cha usajili kutoka Taasisi inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya mwombaji kwenye Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa;
m) Barua ya uthibitisho kuwa Mwombaji ni mwanachama wa Umoja; na
n) Ankra Kifani (endapo mkopo ni wa vitendea kazi).

### 18. Je, Fomu za maombi ya mikopo zinapatikana wapi?

Fomu za maombi ya mikopo zinapatikana katika Tovuti ya Mfuko, Ofisi za Vyama vya Utamaduni na Sanaa na tovuti zao, Ofisi za Maafisa Utamaduni katika ngazi za wilaya na Matawi yote ya Benki za CRDB na NBC

### 19. Je, huchukua muda gani kwa mwombaji kupata Mkopo?

Muda wa kupata mkopo unategemea na ukamilishaji wa nyaraka zinazohitaji kwa ajili ya kupata Mkopo. Muda wa kupata mkopo ni hauzidi siku Ishirini na Moja za kazi (siku 21)

**20. Je, Mwombaji akiwa na Mkataba wa kazi anaweza kupata Mkopo pasipo kuweka dhamana?**

Mwombaji wa mkopo akiwa na mkataba wa kazi anaweza kupata mkopo pasipo kuweka dhamana kwakuwa Mkataba wake unatumika kama dhamana.

**21. Je, Mikopo itolewayo na Mfuko kwa kushirikiana na Benki hutolewa kila baada ya muda gani?**

Hakuna kipindi maalumu cha utoaji wa mikopo, mikopo hii hutolewa muda wote

# SURA YA TATU

## HUDUMA YA MAFUNZO

1. **Je, Mfuko unaprogramu yeyote kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wasanii?**
   Mfuko unasimamia na kuendesha Programu ya Mafunzo ya Urasimishaji wa Kazi za Utamaduni na Sanaa.

2. **Je, Lengo la Programu ya Mafunzo ya Urasimishaji wa Kazi za Utamaduni na Sanaa ni nini?**
   Lengo la Programu ni kuwawezesha wasanii waweze kutekeleza majukumu ya Sanaa katika Mfumo ulio rasmi na kuhudumiwa na mamlaka zilizopo.

3. **Je, Programu hii inajiendesha katika mfumo gani?**
   Programu inajiendesha katika hatua kuu nne ambazo ni:-
   a) Utoaji wa mafunzo kwa wasanii yatakayofanyika kwa muda wa siku mbili;
   b) Uzoefu wa vitendo (Industrial attachement) ambapo msanii ataunganishwa kwa wazalishaji wa sanaa katika eneo lake kwa ajili ya kujifunza zaidi ( Hatua hii inachukua mwezi mmoja);
   c) Ushauri na Ulezi (Mentorship and Coaching) ambapo Msanii ataunganishwa na wasanii wakubwa, wenye uzoefu na wabobezi kwa ajili ya kujifunza mbinu mbalimbali za biashara (Hatua hii inachukua mwezi mmoja); na
   d) Kuunganishwa na fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupata Mkopo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

4. **Je, ni njia gani inayotumika kupata washiriki wa Mafunzo katika Programu hii?**
   Mfuko unapata washiriki kupitia njia zifuatazo:-
   a) Matangazo kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile redio, luninga, magazeti, mitandao ya kijamii nk;
   b) Waombaji wa mikopo ambao maombi yao hayakukidhi vigezo kulingana na Mwongozo wa Mfuko;
   c) Wahitimu wa Vyuo vya Utamaduni na Sanaa vilivyowezeshwa na Mfuko; na
   d) Mashirikisho na Vyama vya Utamaduni na Sanaa.

5. **Je, ni sifa gani zinatumika kwa msanii kujiunga katika Programu hii ya mafunzo?**
   Sifa/Vigezo kwa Msanii kujiunga ni kama ifuatavyo: -
   a) Awe raia wa Tanzania;
   b) Atekeleze kazi ya Utamaduni au Sanaa;

c) Aandike barua ya maombi ya mafunzo na kujaza fomu;
d) Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea;
e) Awe amesajiliwa au kutambuliwa na mamlaka zinazohusika katika utambuzi wa Kazi yake ya Sanaa; na
f) Atambulishwe eneo la makazi na mamlaka husika za Serikali;

### 6. Je, ni fursa/manufaa gani ambayo Msanii anaweza kuzipata baada ya kuhitimu hatua zote za mafunzo katika Programu hii?

Manufaa baada kuhitimu katika Programu ni kama ifuatavyo: -

a) Wanufaika kutunukiwa vyeti;
b) Wanufaika wa Urasimishaji kupata mitaji;
c) Wanufaika kushirikiana na wasanii wakubwa na wenye uzoefu;
d) Kufunguliwa kwa makumpuni na majina ya biashara; na
e) Uwepo wa Mikataba ya ubia kati ya Umma na Sekta Binafsi.

### 7. Je, kuna matarajio gani yanaweza kupatikana kupitia Programu hii?

Yafuatayo ni matokeo kwa wasanii baada ya kuhitimu kwa Programu

a) Kusajili jina la biashara;
b) Kuwa na Mkataba wa pango mahali utakapofanyia biashara;
c) Kuwa na Namba ya Mlipa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
d) Kuwa na leseni ya Biashara kutoka mamlaka husika za Serikali;
e) Kufungua akaunti ya benki kwa ajili ya shughuli za biashara;
f) Kutunza kumbukumbu za mahesabu vizuri ili uweze kupima uhai wa biashara;
g) Kuwa na mikataba ya ajira kama umejiari wafanyakazi;
h) Kukata bima kwa ajili ya kuilinda biashara dhidi ya majanga yasiyotarajiwa mfano, moto, wizi, mafuriko na majanga mengineyo;
i) Kuhudhuria mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara;
j) Kuongeza mtaji wa Biashara kwa kukopa kutoka Taasisi za Fedha.

### 8. Ni nini manufaa ya Programu hii katika Sekta ya Utamaduni & Sanaa na Serikali?

Manufaa ya Programu hii ni kama ifuatavyo:-

k) Kuwezesha Sekta ya Utamaduni na Sanaa iweze kuzalisha ajira kwa wingi nchini hususani katika kundi la vijana;
l) Kuwezesha Sekta ya Utamaduni na Sanaa iwe chanzo kikubwa na endelevu cha kuchangia katika pato la Taifa; na
m) Kuwezesha Sekta ya Utamaduni na Sanaa iwe chanzo kikubwa cha fedha za kigeni kupitia uzalishaji wa bidhaa bora kulingana na mahitaji ya soko la nje ya nchi.

# SURA YA NNE

## MASUALA MTAMBUKA

1. **Je, ni vitu gani muhimu vya kuzingatia kabla ya kuanza usajili wa Kampuni?**
   Ili kuanza hatua za usajili wa Kampuni wahusika wanatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo: -
   a) Namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa watanzania, au nakala ya Hati ya kusafiria kwa raia wa kigeni (Passport);
   b) Anuani ya barua pepe kwa wahusika wote (email addresses);
   c) Namba za simu za kiganjani za wahusika;
   d) Jina la Kampuni;
   e) Anuani ya makazi/ofisi;
   f) Katiba ya kampuni (Memorandum and Articles of Association);

2. **Mahitaji gani yanatakiwa wakati Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara?**
   Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara hutakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-
   a) Cheti cha usajili wa Kampuni (Certificate of Incorporation);
   b) Katiba ya kampuni (Memorandum & Articles of Association) iliyokamilika;
   c) Endapo wenye hisa wa kampuni wote wako nje ya Nchi, Hati ya Uwakilishi (Powers of Attorney) iambatishwe;
   d) Uthibitisho wa mahali pa kufanyia biashara (mf. Mkataba wa pango uliokamilika au Hatimiliki yenye jina la Kampuni inayoomba Leseni;
   e) Hati/Namba ya mlipa Kodi (TIN) ya Kampuni ;
   f) Vitambulisho vya wenye hisa katika Kampuni (mf. Hati ya kusafiria (Passport), Kitambulisho cha Taifa (NIDA), Kitambulisho cha Tanzania cha kupigia kura au cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania);
   g) Kibali cha kuishi nchini daraja la "A" (kwa wenye hisa wasio Watanzania lakini wanaishi Tanzania);
   h) Kibali kutoka kwenye Mamlaka za udhibiti (endapo biashara husika inadhibitiwa na Mamlaka au Sheria maalumu);

3. **Ni mahitaji gani yanatakiwa kuwasilishwa pale mtu binafsi anapotaka kuomba Leseni ya Biashara?**
   a) Kitambulisho, kinachobainisha uraia wa mwombaji;
   b) Uthibitisho wa mahali pakufanyia biashara (Mkataba wa pango uliokamilika au Hatimiliki yenye jina la mwombaji wa Leseni);
   c) Hati/Namba ya Mlipa Kodi (TIN)
   d) Kibali kutoka kwenye mamlaka za udhibiti (endapo biashara husika inadhibitiwa na Mamlaka au Sheria maalumu).

4. **Ni taratibu zipi za kufuata ili kusajili Jina la Biashara?**
Kwanza utatakiwa kufungua Akaunti kwenye mfumo wa usajili (BRELA) kwa njia ya mtandao uitwao Online Registration System (ORS) na kuingiza taarifa za Jina la Biashara.

5. **Ni vitu gani ambavyo vinaweza kumuwezesha Msanii kumiliki Jina la Biashara?**
Kwanza Msanii anatakiwa kuchagua jina litakalotumika katika biashara yako na kusajili ikiwa jina unalotumia kwenye biashara yako halijafanana/ sajiliwa na mtu mwingine basi utasajili na kumiliki jina husika katika biashara yako. Ikiwa jina la biashara limefanana na jina lingine lililosajiliwa na linatumika kwa biashara nyingine basi utatakiwa kubadili jina hilo.

Je, ni vitu gani vinavyozingatiwa katika mfanano wa Majina ya Biashara?
a) Kama yanafanana neno kwa neon;
b) kufanana kwa karibu;
c) Kufanana kwa matamshi mfano skuli na School;
d) Kufanana kwa muonekano; na
e) Kufanana kwa tafsiri Kiswahili / Kiingereza.

6. **Nini maana ya Alama ya Biashara na Huduma?**
Ni alama ya kipekee ambayo imebuniwa na mtu kwa madhumuni ya kutofautisha bidhaa anazozitengeneza au huduma anazozitoa na bidhaa au huduma zinazotolewa na watu wengine wanaotengeneza bidhaa au kutoa huduma zinazofanana na za kwake. Alama ya Biashara au Huduma inaweza kuwa neno, umbo, mchoro, nambari, kifupi cha jina halisi au jina bunifu la mmiliki, kampuni au jina/neno la kubuni isipokuwa yale ambayo yamekatazwa kisheria

7. **Ni vigezo gani ambavyo vinahitajika ili kupata Alama ya Biashara au Huduma?**
a) Alama iwe ya kipekee ambayo amebuniwa na mmiliki mwenyewe;
b) Alama hiyo isifanane na alama ambayo ilishasajiliwa na mtu mwingine katika daraja husika;
c) Isiwe na sifa za bidhaa au huduma husika daraja husika; na
d) Isiwe kinyume cha sheria na maadili ya Kitanzania.

8. **Ni taratibu zipi za kufuata ili kusajiliwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)?**
Kwanza utatakiwa kufungua Akaunti kwenye mfumo wa usajili (BASATA) kwa njia ya mtandao uitwao Application Management Information System (AMIS) kupitia "Sanaa.go.tz" na kuingiza taarifa za kazi Sanaa unazofanya.

9. **Je, mahitaji gani yanahitajika ili Msanii binafsi aweze kusajiliwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Msanii binafsi BASATA:-

a) Kitambulisho cha Taifa/Hati ya Kusafiria/Cheti cha kuzaliwa/ Kitambulisho cha mpiga Kura /Leseni ya Udereva;
b) Picha (Passport size); na
c) Wasifu (Biography) wa Msanii inayomuonesha Sanaa anayoifanya.

10. **Je, mahitaji gani yanahitajika ili Kikundi kiweze kusajiliwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Kikundi BASATA:-

a) Katiba ya Kikundi;
b) Picha za viongozi wa Kikundi;
c) Muhtasari wa kikao; na
d) Orodha ya wanachama wa Kikundi.

11. **Je, mahitaji gani yanahitajika ili Kampuni iweze kusajiliwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Kampuni BASATA:-

a) Katiba ya kampuni (Memorandum and Article of associations);
b) Picha za viongozi wa Kampuni;
c) Muhtasari wa kikao;
d) Orodha ya wanachama wa Kampuni; na
e) Uthibitisho wa usajili kutoka BRELA.

12. **Ni taratibu zipi za kufuata ili kusajiliwa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB)?**

Kwanza utatakiwa kufungua Akaunti kwenye mfumo wa usajili (Bodi ya Filamu Tanzania) kwa njia ya mtandao uitwao Application Management Information System (AMIS) kupitia "sanaa.go.tz" na kuingiza taarifa zako za Biashara ya kazi ya Filamu.

13. **Je, mahitaji gani yanahitajika ili Msanii binafsi aweze kusajiliwa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB)?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Msanii binafsi Bodi ya Filamu Tanznia:-

a) Kitambulisho cha Taifa/Hati ya Kusafiria/Cheti cha kuzaliwa/ Kitambulisho cha mpiga Kura /Leseni ya Udereva; na
b) Picha (Passport size) ya Msanii;

14. **Je, mahitaji gani yanahitajika ili Kikundi kiweze kusajiliwa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB)?**

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Kikundi Bodi ya Filamu Tanzania:-

a) Fomu ya usajili kutoka Bodi ya Filamu Tanzania;
b) Leseni ya biashara ya Filamu;
c) Katiba ya Kikundi; na
d) Orodha ya majina ya wanachama wa Kikundi.

### 15. Je, mahitaji gani yanahitajika ili Kampuni iweze kusajiliwa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB)?

Mahitaji yafuatayo yanakamilisha usajili wa Kampuni Bodi ya Filamu Tanzania:-

a) Leseni ya Kampuni inayojihusisha na Filamu;
b) Uthibitisho wa usajili kutoka BRELA; na
c) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN).

**Kimeandaliwa na:**
Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania
Jengo la Utumishi, Block, A, 8 Barabara yaKivukoni,
S.L.P 8031, 11101 KIVUKONI,
**DAR ES SALAAM**

**Simu:** 0738 246 286

mfukotamadunits www.tacaf.go.tz

mfuko.utamaduni@michezo.go.tz